**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

**Tovuti: www.hlpc.go.tz**

# TANGAZO

## MATOKEO YA MTIHANI WA USAJILI ULIOFANYIKA APRILI 2024

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara linapenda kuwataarifu Wataalam wa maabara waliofanya mtihani wa usajili mwezi Aprili 2024 kuwa matokeo ya Mtihani huo yametoka leo tarehe 16.05.2024

Matokeo ya kila mtahiniwa yamewekwa kwenye akaunti ya mmoja ya mfumo wa ***hprs.moh.go.tz***. Ili Mtahiniwa aweze kuona matokeo yake anatakiwa kuingia kwenye akaunti yake kipengele cha ***examination application*** halafu aende sehemu ya ***complete application***

Watahiniwa wote waliofaulu mitahani yao wanatakiwa kuomba usajili wa kudumu mapema kabla ya tarehe 30.06.2024. Waombaji wote wa usajili wa kudumu na kuorodhesha wanatakiwa wahakikishe wameambatanisha nyaraka zifuatazo ili maombi yao yaweze kushughulikiwa;

- Cheti cha Kuzaliwa
- Cheti cha Kidato cha nne au cha sita
- Cheti cha Chuo (Kisiwe ***leaving certificate***)
- Cheti cha Matokeo ya Chuo (Academic Transcript)
- Cheti cha Utibitisho kutoka NACTVET au TCU kwa waliosoma vyuo vya nje ya nchi
- Wasifu (CV)

Aidha, Dirisha la maombi ya usajili **litafunguliwa tarehe 16.05.2024** na **kufungwa tarehe 30.06.2024.** Wote waliofaulu wanasisitizwa kufanya maombi ya usajili wa kudumu au kuorodheshwa kabla ya dirisha kufungwa.

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara linawatakia utekelezaji mwema

Kwa msaada zaidi piga simu 0734005777

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
16.05.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
16 MAY 2024
P.O.Box 743
DODOMA